

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA**



**WITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MFUMO WA SHERIA YA HUDUMA ZA USTAWI WA  
JAMII NCHINI**

---

**1.0 Utangulizi**

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto hivi sasa inafanya Utafiti kuhusu Mfumo wa Sheria ya Huduma na Ustawi wa Jamii Nchini. Madhumuni ya utafiti ni kupata maoni na mapendekezo ya wananchi, wadau na taasisi mbalimbali yatakayoweza nchi yetu kuwa na mfumo madhubuti wa kisheria wa kuratibu utoaji wa huduma za jamii na kudhibiti na kusimamia taaluma ya ustawi wa jamii. Umuhimu wa kuratibu na kurtibu utoaji wa huduma na udhibiti wa taaluma ya ustawi wa jamii hivi sasa ni jambo nyeti na lazima kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili kwa watoto, wanawake na wazee vinavyosabishwa na mmomonyoko wa maadili, kuvunjika kwa ndoa na kusambaratika kwa familia, ajira kwa watoto, biashara ya binadamu, matumizi ya madawa ya kulevya kwa vijana, magonjwa yasiyotibika na kadhalika.

**2.0 Madhumuni ya Utafiti**

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 8(1) na (2) cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171, utafiti una malengo makuu yafuatayo:-

- (i) Kuimarisha mfumo uliopo wa sheria za huduma za ustawi wa jamii ili kuboresha huduma hizo;
- (ii) Kuangalia uwezekano wa kupendekeza mfumo mpya wa sheria utakaosimamia taaluma ya ustawi wa jamii; na
- (iii) Kuishauri Serikali namna ya kuboresha sera mbalimbali zenye malengo ya kukuza huduma za ustawi wa jamii nchini.

Baada ya kukamilisha utafiti, Tume itawasilisha taarifa yenye mapendekezo yatakayokidhi mahitaji ya sekta ya ustawi wa jamii na taaluma ya utoaji wa huduma kwa jamii.

### **3.0 Maoni na Mapendekezo ya Wananchi**

Ili kuwezesha kufanyika kwa utafiti huo kikamilifu na, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10(1) (2) cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171, Tume inatoa wito kwa watu binafsi, taasisi za Serikali na binafsi kushiriki katika kutoa maoni na mapendekezo kuhusu namna bora ya kukuza na kuiboresha sekta ya ustawi wa jamii na taaluma ya utoaji wa huduma kwa jamii.

### **4.0 Muda wa Kupata Maoni/Mapendekezo**

Ili kukamilisha utafiti huu mapema, Tume imeweka muda wa siku **30** kuanzia tarehe **12/11/2017** hadi tarehe **12/12/2017** kupata maoni na mapendekezo kutoka kwa wananchi, wadau na taasisi husika.

### **5.0 Namna ya Kutuma Maoni/Mapendekezo**

Maoni na Mapendekezo yanaweza kuwasilishwa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kupitia njia zifuatazo:

#### **Anuani ya barua**

Katibu Mtendaji,  
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,  
Jengo la Haki, Mtaa wa Luthuli,  
S.L.P. 3580,  
**DAR ES SALAAM**

#### **Simu ya Mezani**

Simu: +255 22 2123533/2111387

#### **Barua pepe**

lrct@lrct.go.tz

#### **Mtandao wa Kijamii**

[www.facebook.com/tumesheria.tanzania](http://www.facebook.com/tumesheria.tanzania)

#### **Tovuti**

[www.lrct.go.tz](http://www.lrct.go.tz)

Imetolewa na:



Casmir S. Kyuki

**KATIBU MTENDAJI**